

TAARIFA YA MAFUNZO YA PS3 KUHUSU KOBORESHA TOVUTI ZA SERIKALI ZAMITAA KWA MAAFISA HABARI NA MAAFISATEHAMA

1. Utangulizi

Ofisi ya katibu Mkuu TAMISEMI imeandaa mafunzo ya maboresho ya tovuti za serikali katika mradi wa PS3 unaofadhiliwa na USAIDs yaliyofanyika Mkoani mbeya kwa kuwahusisha wataalamu wa Habari na TEHAMA kwa muda wa siku tano. Awali mafunzo hayo yalikuwa yafanyike kuanzia tarehe 26/3/2018 lakini yaliahirishwa na kufanyika kuanzia tarehe 9/10/2018 katika ukumbi wa Usungilo ulioko Mjini mbeya

Halmashauri ya Mlele iliwakililishwa na wataalam wawili ambaoni Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA na Msaidizi wa mambo ya Habari Abasi Issa Chimsala ambao walihudhuria muda wote wa mafunzo “Workshop”.

2. Lengo la Mafunzo

Lengo la mafunzo ni kupata uelewa kuhusu muongozo wa Matumizi ya Tovuti na kuboresha muonekana wa Tovuti zote za Serikali na kuzifanya kuwa na muonekano unaofanana.

3. Mambo Muhimu Yaliyoelekezwa

Katika Mafunzo hayo maelekezo mengi yanatoka katika Muongozo wa matumizi ya Tovuti za serikali ambao unaeleza kwa kina matumizi ya tovuti hizo katika serikali za mitaa na taasisi zingine za serikal.

4. Changamoto Zilizopo Katika Kutekeleza Maagizo ya Tovuti

- Uhaba wa watumishi wa kada za TEHAMA na Uhusiano ambapo uchache huo unasababisha mtu mmoja kufanya kazi ya zaidi ya mtu mmoja.
- Idara tumizi kutokuwa na muamko wa kutumia tovuti za serikali aidha kwa sababu za kutokuwa na elimu ya matumizi ya tovuti ama Internet.
- Ukosefu wa mtandao wa Inernet ambapo halmashauri yetu haina Mtandao wa Internet hivyo ni changamoto kwa wakuu wa idara, vitengo na watumishi wa Idara kufuatilia tovuti yetu.

- Muamko wa watu nje ya Halmashauri kutumia tovuti ili kupata taarifa mbalimbali na kupata habari zinazohusu maendeleo yao.

5. Mikakati ya kutatua Changamoto

- i. Kwa muda ambao Halmashauri infanya jitihada kupata watumishi wa kada hizo tutaendelea kushirikisha watumishi kada zingine kusaidia kazi na pia kuwatumia wanao jitolea katika kadi hizi
- ii. Kingo kitaendelea kutoa elimu ya uelewa kwa wadau wa Tovuti za serikali hususani katika halmashauri yetu ya Mlele.
- iii. Kutumia mitandaomingine ya kijamii kuitangaza tovuti yahalmashauri ya Mlele www.mleledc.go.tz kama vile whatsapp, facebook, Youtube na Twita
- iv. Kufunga mtandao wa internet ya Wifi katika ofisi zote za halmashauri zitakazo tumika kwa watumiaji wenye akaunti na Mnywila(password) tu.
- v. Kuweka Habari nyingi katika tovuti zinazovutia ili kuhakisha tovuti yetuinakuwa kiini kikubwa habari na taarifa kwa watumishi na Umma kwa ujumla.

6. Ushauri na mapendekezo ya kuifanya Tovuti yetu iwe Bora

- Kila Mkuu wa Idara ahakikishe kurasa zote zinazo mhusu zina Taarifa nzuri inayohitajika kwa kuiandaa na kuiwasilisha TEHAMANA Mahusiano ipandishwe kwenye tovuti.
- Kumtumia Afisa habari/TEHAMA katika matukio yote yanayohusu halmashauri yetu na kuhakikisha matukio hayo yamepandishwa kwenye Tovuti.
- Kuipandisha miradi yote ya Halmashauri katika Tovuti na nyaraka zote muhimu zinahitajika kwa wananchi na Watumishi wa halmashauri.
- Kuwa na interneti itakayotumika katika kompyuta za Halmashauri ili watumishi waweze kupata namna ya kutumia tovuti ya Halmashauri na kupata habari.
- Kutoa matangazo yote ya Halmashauri kupitia tovuti zetu na kutumia liunganishi cha kurasa kwenye mitandao ya kijamii. Kabla ya kupeleka tangazo popote lipandishwe katika Tovuti.

7. Mwisho

Hakuna wa kuweza kuuonyesha umma uwezo wako wa kufanya kazi na kuitangaza Halmashauri yetu kama hutaona umuhimu wa kujitangaza kwa kazi zako kwa kuitumia vema tovuti ya Halmashauri yetu

Joseph Peter Mkumbwa
KAIMU MKUU KITENGO CHA TEHAMA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE